# JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM

# PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO



# KALENDA YA MAADHIMISHO NA MATUKIO

# 2025



# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM

## PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO



S.L.P. 280 D'SALAAM, E: katolikimshikamano@gmail.com

### PAROKIA NA UONGOZI

Parokia ya Kung'ara kwa Yesu Kristo, Mbezi Mshikamano ilitangazwa kuwa Parokia kamili na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Mwadhama Polycarp Kardinali Pengo tarehe 26.04.2016 na Misa ya kwanza 01.05.2016. Parokia inasimamiwa na Mapadre wa Shirika la Wamisionari wa Africa (M.Afr.), kati ya Mashirika matatu ya kwanza kuinjilisha nchini Tanzania. Awali msimamizi wa Parokia alikuwa Mt. Yohane Paulo II mpaka siku ya Kutabaruku Kanisa la Parokia katika sikukuu ya Kung'ara kwa Yesu Kristo, 06.08.2023 ambapo Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la D'Salaam, Mhashamu Jude Thaddaeus Ruwa'ichi alibadilisha msimamizi kuwa Kung'ara kwa Yesu Kristo. Paroko wa kwanza alikuwa Pd. Bartholomew Mrosso (M.Afr) (2016-2018), akifuatiwa na Pd. Francis Kangwa (M.Afr) kuanzia 20.06.2018 hadi 13.04.2022 alipofariki dunia (*Bwana ampe pumziko la milele*). Pd. Louis Ntamati (M.Afr.) (*Kaimu*) kuanzia 15.04.2022 - 05.02.2023 na Paroko, Pd. Gilbert Bujiriri (M.Afr.) kuanzia 05.02.2023 - 25.06.2023. Paroko, Pd. Protogene Rugwizandekwe (M.Afr) kuanzia 25.06.2023 akisaidiwa na Pd. Francis Xavier Angkosaala (M.Afr) na Pd. Venance Bharotota (M.Afr) mpaka Julai 2024. Pd. Gilbert Bujiriri kuanzia Julai 2024 akisaidiwa na Pd. Venance na baadaye Pd. Theodore Ouedraogo (14.11.2024) na Pd. Jean Paul Basikaba Evi (Aprili 2025). Parokia ina familia 642, waamini wote 2,807.

### HALMASHAURI YA WALEI (2023-2026)

Halmashauri ya Walei inaundwa na Jumuiya 39 zilizogawanywa katika Kanda 11. Kamati Tendaji ya Halmashauri ya Walei Parokia iliyochaguliwa 19.02.2023 ni:

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti: | Adam Kamanda |
| Makamu M.kiti: | Alfred Tarimo |
| Katibu: | Silvani Mng'anya |
| Katibu Msaidizi: | Vitalis Mruma |
| Katibu Msaidizi: | Alphonsina Ndunguru |
| Mtunzahazina: | Eva Mushi |

### SALA KATIKA JUMUIYA NA KANDA

Mikutano ya sala katika Jumuiya hufanyika kila Jumamosi saa 12:30 asubuhi na mikutano ya sala katika Kanda kila Jumamosi ya tatu ya mwezi, na ikiwepo sababu ya kubadilisha itatangazwa kwa wakati. Kila Jumuiya na Kanda inahimizwa kuadhimisha Misa kwa heshima ya wasimamizi wao.

### MISA PAROKIANI NA KUABUDU EKARISTI TAKATIFU

Siku za Dominika huadhimishwa Misa tatu, saa 12:30, saa 2:30 asubuhi na Misa ya watoto saa 5:00 asubuhi. Siku za sherehe na sikukuu au matukio muhimu utaratatibu utatangazwa. Siku za wiki Jumatatu hadi Ijumaa Misa Takatifu huadhimishwa saa 12:30 asubuhi zikitanguliwa na masifu saa 12:00 asubuhi. Siku za Alhamisi ibada ya kuabudu Ekaristi Takatifu saa 11:00 jioni na kipindi cha Kwaresma siku za Ijumaa Njia ya Msalaba saa 10:30 jioni ikifuatiwa na Misa Takatifu. Kila Jumamosi ya kwanza ya mwezi inaadhimishwa Misa kwa heshima ya Moyo Safi wa Bikira Maria, saa 3:00 asubuhi baada ya sala za Jumuiya.

### SAKRAMENTI

Sakramenti ya ubatizo hutolewa kila Dominika ya mwisho wa mwezi katika Misa ya pili. Sakramenti ya Kitubio hutolewa kila Alhamisi wakati wa kuabudu na siku za wiki baada ya Misa za asubuhi na kila mwaamini anapohitaji upatanisho anaweza kumuomba Padre. Wagonjwa wanahudumiwa Ekaristi Takatifu siku za Alhamisi na Dominika au pale inapohitajika kupitia Mapadre au Wahudumu wa Ekaristi Wasio wa Kawaida.

**Kuandikisha ndoa:**

Kila Ijumaa kuanzia saa 8.00 mchana.

### HUDUMA YA OFISI

| SIKU | ASUBUHI 3:00 - 6:00 | MCHANA 6:00 - 9:00 | JIONI 9:00 -11:00 |
|---|---|---|---|
| JUMATATU | MAPUMZIKO | MAPUMZIKO | MAPUMZIKO |
| JUMANNE HADI IJUMAA | HUDUMA | MAPUMZIKO | HUDUMA |
| JUMAMOSI | MISA ZA JNNK | MAPUMZIKO | MISA ZA JNNK |

Siku za Jumamosi zimetengwa kwa ajili ya Misa za wasimamizi wa Jumuiya na Kanda na matukio ya mafungo na Hija. Jumamosi za kwanza za mwezi inaadhimishwa Misa kwa heshima ya Moyo Safi wa Bikira Maria.

### VYAMA, MASHIRIKA NA JUMUIYA ZA KITUME (VMJ)

Parokia ina Vyama, Mashirika na Jumuiya za Kitume (VMJ) kumi na tano. Vyama na mashirika hayo ni: Utume wa Wanaume Katoliki (UWAKA), Wanawake Wakatoliki Tanzania (WAWATA), Vijana Wafanyakazi Wakatoliki (VIWAWA), Utume wa Wazee na Wastaafu wa Mt. Augustino, Shirika la Kipapa la Utoto Mtakatifu (wakilelewa na WAWATA), Utume wa Kwaya Katoliki Tanzania (UKWAKATA Parokia), Ushirika wa Moyo Mtakatifu wa Yesu, Mt. Vinsenti wa Paulo, Shirika la Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili, Shirika la Mt. Alois Gonzaga (Watumishi wa Altare), Lejio ya Maria, Wanataaluma Wakristo Tanzania (Christian Professionals of Tanzania – CPT), Karismatiki Katoliki, Utume wa Familia Katika Kristo (Couples For Christ - CFC), na Chama cha Upendo cha Mt. Theresia wa Mtoto Yesu. Matarajio ya mwaka 2025 ni kuanzisha Utume wa Rozari Hai, Scout Katoliki, na Utume wa Wajane na Wagane. Aidha, Marafiki wa Wamisionari wa Afrika (Undugu Association) unafanya utume wake kwa sala, semina, mafungo na kuwaombea mapadre na watawa.

### VIKAO NA MIKUTANO

Vikao vya Kamati Tendaji Parokia hufanyika kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi saa 12:00 jioni. Mikutano ya Halmashauri ya Walei Parokia hufanyika kila baada ya miezi mitatu baada ya Misa ya kwanza. Vyama, Mashirikana Jumuiya za Kitume (VMJ) vinahimizwa kufuata ratiba ya vikao na mikutano kadiri ya Kanuni na Kalenda zao.

### MAFUNDISHO

**Ekaristi (Komunio ya Kwanza) na Kipaimara** ni kila Jumamosi saa 3:00 - 5:00 asubuhi; Jumatatu na Jumatano saa 10:00 – 11:30 jioni.
**Wakatekumeni**: Kila Ijumaa saa 3:00 asub. – 6.00 mchana.
**Semina za ndoa**: Kutegemea mahitahi na upatikanaji wa wahusika.
Mafundisho ya Dini Baada ya Kipaimara (**MADIBAKI**) – Utaratibu na ratiba kamili itatolewa.

### SEMINA, MAFUNGO NA HIJA

Ili kuhuisha imani Parokia itaandaa Semina, Hija na mafungo kwa makundi, mashirika na vyama vya kitume hasa kwa vipindi maalum vya Kanisa kama Majilio, Kwaresma, Pasaka, na wakati ufaao. Pia semina za pamoja kwa waamini wote zitaandaliwa na kufanyika katika Dominika moja hasa ya tatu ya mwezi.

### KAMATI ZA KIKATIBA NA KITAALUMA

**Kamati za Kikatiba**: 1. Malezi, Familia na Afya; 2. Maadhimisho, Ibada na Liturujia; 3. Haki, Amani, Ulinzi na Usalama; 4. Elimu ya Dini, Mafundisho ya Kanisa na Teolojia; na 5. Mipango, Uchumi na Fedha.
**Kamati za Kitaaluma**: 1. Kamati ya Ufundi na Ujenzi; 2. Kamati ya Uinjilishaji; 3. Kamati ya Zaka; 4. Kamati ya Afya; 5. Kamati ya Ardhi na Mazingira; 6. Kamati ya Sheria; 7. Kamati ya Ndoa na Familia, 8. Kamati ya Habari na Mawasiliano; 9. Kamati ya Sherehe, 10. Kamati ya Ulizi na Usalama, na 11. Kamati ya Mavuno.

## UJENZI

Kazi kubwa ya ujenzi wa Kanisa na Nyumba ya Mapadre unaoendelea Parokiani unawezeshwa na waamini wa Parokia kupitia michango binafsi ya kila mwezi lakini ikiwasilishwa kila wiki, Mchango wa Maendeleo. Mchango huu unashindanishwa kijumuiya na majumuisho kufanyika kila Dominika ya kwanza ya mwezi unaofuata. Shughuli za Ujenzi zinasimamiwa na Kamati ya Ujenzi na Ufundi. Pesa yote inayochangwa inaingizwa (*iingizwe*) katika akaunti za Parokia ikionesha lengo na mwekaji.

1. **Parokia ya Kung'ara kwa Yesu Kristo, Benki ya CRDB**, namba: **015C568083000, Tawi la Mbezi Luis**

2. **Parokia ya Kung'ara kwa Yesu Kristo**, Namba **00111509088101**, **Benki ya Biashara ya Mkombozi, Tawi la St. Joseph.**

## ZAKA

Zaka (asilimia kumi (10%) ya pato la mwaamini) ni agizo la Mungu na Amri ya Tano ya Kanisa, **Saidia Kanisa Katoliki kwa Zaka**.

- Fungu la kumi ….. Kumbukumbu la Torati 14:22
- Sehemu ya kumi…… Waebrania 7:5
- Zaka …… Mambo ya Walawi 27:32

Waamini wote wanahimizwa kutoa zaka kadiri Mungu alivyowajalia ili kupata baraka zilizoahidiwa na Mungu Mwenyewe…. (Malaki 3:10) *"Leteni zaka kamili ghalani, ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanijaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha."*

Kila mwaamini anatakiwa kujisajili katika mfumo wa Zaka *digitali* na kulipa kwa zaka kwa uaminifu. Namba ya zaka ya Parokia ni **SAS525**….

## WAHITAJI

Parokia inao utaratibu wa kuwahudumia baadhi ya wahitaji walio ndani ya eneo la Parokia bila kujali imani zao. Kupitia mchango wa waamini Kanisani, michango binafsi ya vitu na pesa hugawiwa mara moja kila mwezi (Jumanne baada ya Dominika ya mwisho wa mwezi), na katika sherehe za Noeli na Pasaka. Huduma hutolewa kupitia chama cha Mt. Vinsenti wa Paulo (*St. Vincent de Paul*). Pia ipo akaunti maalum ya kusaidia mfuko huu, unaweza kuchangia kupitia hiyo:

**St. Vicent Mbezi Mshikamano,** Namba **00111509088103,**
**Benki ya Biashara ya Mkombozi, Tawi la St. Joseph**

Mathayo 25:35-40 …"Kwa maana mmojawapo wa hao ndugu zangu walio wadogo alipokuwa na njaa, kiu, mgeni, uchi, mgonjwa, na kifungoni mkamhudumia, mlinitendea mimi."

## NYUMBA YA MALEZI YA WAMISIONARI WA AFRIKA

Nyumba ya Malezi (Formation House) ya Shirika la Wamisionari wa Afrika (M.Afr) iliyo jirani na Parokia imetoa mchango mkubwa kwa Parokia tangu ilipoanza kama Kanisa Dogo na Kigango, wakati wa maandalizi na ujenzi wa Kanisa katika hatua za mwanzo. Waamini walianza kusali katika Nyumba hiyo ya Malezi wakati huo (2009 - 2014).

Hata baada ya ujenzi wa Kanisa na kutangazwa kuwa Parokia (2016), ushirikiano umeendelea ikiwepo vijana wa Malezi (Mafrateri) kushiriki mikutano ya sala za Jumuiya, na Vyama vya Kitume, na Mapadre kushiriki Maadhimisho ya Misa na matukio mengine Parokiani. Ushirikiano huu ni muhimu katika kuujenga Mwili wa Kristo – Kanisa Moja Takatifu la Mitume!

***Jubilei 2025…. Mahujaji wa Matumaini!***

| JANUARI 2025 - Jina Takatifu la Yesu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumapili | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi |
| | | | 1<br>Sherehe ya Bikira Maria Mama wa Mungu | 2<br>Mt. Basili Mkuu | 3<br>Jina Takatifu la Yesu | 4<br>Misa ya Ushemasi |
| 5<br>Sherehe ya Tokeo la Bwana, Epifania | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 |
| 12<br>Sikukuu ya Ubatizo wa Bwana<br>Mkutano Mkuu UFATA (J)<br>Mapinduzi Z'bar | 13 | 14 | 15<br>Kuanza Kozi ya UFATA (J) P1 | 16 | 17 | 18<br>Kumbukumbu ya Wamisionari Pugu |
| 19<br>Dominika ya 2: Mwaka C | 20 | 21<br>Mt. Agnes | 22 | 23 | 24<br>Kamati Tendaji Dekania<br>**Jubilei Kuu**: mawasiliano, vyombo vya habari (24-26.01) | 25<br>Sikukuu ya Kuongoka kwa Mt. Paulo Mtume |
| 26<br>Dominika ya 3: Mwaka C - Neno la Mungu<br>Kikao cha Utendaji Viongozi Dekania, Kamati (J)<br>Mt. Timotheo | 27 | 28<br>Mt. Thomas wa Akwino | 29 | 30 | 31<br>Mt. Yohane Bosko | |

| FEBRUARI 2025 – Familia Takatifu na Ndoa | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | | | | | | **1**<br>Sikukuu/ Jubilei ya Watawa<br>Kikao cha Utendaji viongozi VMJ (J) |
| **2**<br>Sikukuu ya Kutolewa Bwana Hekaluni | **3** | **4** | **5**<br>Mt. Agatha | **6** | **7** | **8**<br>**Jubilei Kuu**: Majeshi, polisi, vyombo vya usalama (08-09.01) |
| **9**<br>Dominika ya 5: Mwaka C<br><br>**Mkutano HW Parokia** | **10**<br>Mt. Skolastika | **11**<br>Bikira Maria wa Lurdi<br>Kuombea wagonjwa/ wahudumu afya | **12** | **13** | **14**<br>Wat. Sirili na Metodi | **15**<br>Misa ya shukrani – Wazee na wastaafu (J), Wajane na Wagane<br>**Jubilei Kuu**: Wasanii na wanamichezo (15-18.01) |
| **16**<br>Dominika ya 6: Mwaka C | **17** | **18** | **19** | **20** | **21**<br><br>**Jubilei Kuu**: Mashemasi (21-23 Feb) | **22**<br>Sikukuu ya Ukulu wa Mt. Petro Mtume |
| **23**<br>Dominika ya 7: Mwaka C | **24** | **25** | **26** | **27** | **28** | |

| MACHI 2025 - Mt. Yosefu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | | | | | | **1** |
| **2**<br>Dominika ya 8: Mwaka C | **3** | **4** | **5**<br>Jumatano ya Majivu | **6**<br>Kamati Tendaji Dekania | **7**<br>Kuundwa Jimbo jipya la Bagamoyo<br>Mt. Perpetua, Mt. Felista | **8**<br>Hija na Mafungo HW (J), Pugu |
| **9**<br>Dominika ya 1: Kwaresma C | **10** | **11** | **12** | **13** | **14** | **15** |
| **16**<br>Dominika ya 2: Kwaresma C | **17** | **18** | **19**<br>Sherehe Mt. Joseph, Mume B. Maria, Msimamizi Jimbo | **20** | **21**<br>Mafungo, mkesha (Moyo Mt. Yesu) | **22**<br>Mafungo WAWATA (Parokia) |
| **23**<br>Dominika ya 2: Kwaresma C | **24** | **25**<br>Kupashwa Habari ya Kuzaliwa Bwana | **26** | **27** | **28**<br>Mkesha, mafungo UWAKA (J)<br>28-03.03 Mafungo Karismatiki | **29**<br>Hija VIWAWA (J)<br>Mafungo (Wajane & Wagane) |
| **30**<br>Dominika ya 4: Kwaresma C<br>Mkutano Mkuu HW (J) | **31**<br>Iddi Elfitri 1<br>Mafungo ya wtoto (Par) | | | | | |

| APRILI 2025 – **Huruma ya Mungu** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| Kupokea sanamu ya Bikira Maria katika safari ya Mahujaji wa Matumaini na **Utume wa Rozari Hai,** 05.04 kutoka Tegeta A na kukabidhi 22.04 Kibamba | | **1**<br>Iddi Elfitri 2<br>Mafungo wa Kwaresma Parokia | **2** | **3** | **4** | **5**<br>Hija, Mafungo UFATA (J)<br>**Jubilei Kuu**: Wagonjwa, wahudumu afya<br>Sanamu B. Maria R. Hai |
| **6**<br>Dominika ya 5: Kwaresma<br>Utambulisho wa mafundisho ya UFATA (Parokia) | **7**<br>Karume Day | **8** | **9** | **10** | **11** | **12**<br>Mafungo WAWATA (J)<br>Mafungo ya Vijana (Par) |
| **13**<br>Dominika ya Matawi: Mateso C | **14** | **15**<br>Misa ya Krisma, kubariki Mafuta Matakatifu<br>Mt. Bernadeta | **16** | **17**<br>Alhamisi Kuu | **18**<br>Ijumaa Kuu | **19**<br>Jumamosi Kuu (Vijilia ya Pasaka) |
| **20**<br>**Sherehe ya Pasaka** | **21**<br>Jumatatu ya Pasaka<br>Misa UKWAKATA (J) | **22**<br>Kukabidhi sanamu ya B. Maria | **23** | **24** | **25**<br>Sikukuu Mt. Marko Mwinjili<br>**Jubilei Kuu**: Vijana chini ya miaka 20 (25-27.04) | **26**<br>Muungano |
| **27**<br>Dominika ya 2 ya Pasaka - Huruma ya Mungu | **28**<br>**Jubilei Kuu**: Watu wenye ulemavu | **29**<br>Mt. Katarina wa Siena<br>Kumuaga Askofu Musomba (J) | **30** | | | |

| MEI 2025 - Mama Bikira Maria | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | | | | **1**<br>Mt. Yosefu Mfanyakazi<br>**Jubilei Kuu**: Wafanyakazi, wajasiriamali, wamachinga (1-11 Mei) | **2** | **3**<br>Wat. Filipo na Yakobo, Mitume<br>Semina za Dekania HW (J)<br>Kumsindikiza Askofu Musomba Jimbo jipya la Bagamoyo |
| **4**<br>Dominika ya 3 ya Pasaka<br>Kuzinduliwa Jimbo jipya la Bagamoyo | **5** | **6** | **7** | **8**<br>Kamati Tendaji Dekania<br>Kuchaguliwa Papa Leo XIV | **9** | **10**<br>UWAKA Day (J), Pugu |
| **11**<br>Dominika ya 4 ya Pasaka – Mchungaji Mwema, MIITO | **12** | **13** | **14** | **15**<br>Mt. Isdori Mkulima | **16**<br>Mt. Simon Stock | **17**<br>Kikao cha utendaji viongozi Dekania, Kamati (J) |
| **18**<br>Dominika ya 5 ya Pasaka, C | **19** | **20** | **21** | **22**<br>Mt. Rita wa Kashia | **23** | **24**<br>Kikao cha utendaji viongozi VMJ (J) |
| **25**<br>Dominika ya 6 ya Pasaka, C<br>Mt. Gregory VII | **26** | **27** | **28** | **29**<br>Siku 40 baada ya Ufufuko wa Bwana | **30**<br>Kuanza Novena ya Roho Mtakatifu<br>**Jubilei Kuu**: Familia, Watoto, Mabibi, Mababu na Wazee (30.05-01.06) | **31**<br>B. Maria kumtemb. Elizabeti<br>Kumuombea Askofu Mkuu kidekania (saa 10)<br>**Pugu Marathon** |

| JUNI 2025 - Moyo Mtakatifu wa Yesu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| **1**<br>Sherehe ya Kupaa Bwana<br>Mweny. Antonio Rosmini | **2** | **3**<br>Wat. Mashahidi wa Uganda....<br>Mt. Mathias Mulumba, Mt. Kizito, Mt. Yohane Maria Muzeey | **4** | **5** | **6**<br>Kamati Tendaji Dekania | **7** Iddi<br>**Jubilei Kuu**: Vyama ya Kitume, 07-08 Juni)<br>Hija na Mafungo VMJ Jubilei Kuu, Pugu<br>Kesha la Pentekoste |
| **8**<br>Sherehe ya Pentekoste<br>**Mkutano HW Parokia** | **9**<br>Bikira Maria Mama wa Kanisa | **10** | **11**<br>Sikukuu Mt. Barnaba, Mtume | **12** | **13**<br>Mt. Antoni wa Padua | **14**<br>Halmashauri Walei Dekania - Msakuzi |
| **15**<br>Sherehe ya Utatu Mtakatifu | **16** | **17** | **18** | **19** | **20**<br>20.06 – 06.07<br>Kongamano la Roho Mtakatifu<br>**Jubilei Kuu**: Viongozi wa serikali (20-22.06) | **21**<br>**Semina ya Kamati ya Uinjilishaji (Parokia)**<br>Kipaimara Makabe |
| **22**<br>Sherehe ya Mwili na Damu ya Bwana Wetu Yesu Kristo, Ekaristi Takatifu | **23**<br>Mafungo kujiandaa na sherehe Moyo Mt wa Yesu<br>**Jubilei Kuu**: Waseminari (23-24 Juni) | **24**<br>Sherehe ya Kuzaliwa Mt. Yohane Mbatizaji | **25**<br>**Jubilei Kuu**: Mapadre (25-27 Juni) | **26**<br>Hija Pugu, Ujasiriamali Upendo Group | **27**<br>Sherehe ya Moyo Mtakatifu wa Yesu<br>- Bikira Maria Consolata | **28**<br>Hija - heshima ya Moyo safi wa Maria, Pugu<br>Kipaimara Mbezi Louis |
| **29**<br>Sherehe ya Wat. Petro na Paulo Mitume | **30** | | | | | |

| JULAI 2025 - Damu Takatifu ya Yesu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| Kozi ya Uimarishaji wa Familia (UFATA), 1-31 Julai, Kituo cha Walei, Isidori Bakanja, Stakishari, Dar es Salaam | | **1** Sikukuu ya Damu Azizi ya Yesu | **2** | **3** Sikukuu ya Mt. Toma, Mtume | **4** | **5** **Hija na Mafungo Parokia, Padre Pio Shrine** |
| **6** Dominika ya 14: Mwaka C Mt. Maria Goretti | **7** Saba saba - Biashara Sherehe ya Upadrisho | **8** | **9** | **10** | **11** Mt. Benedikto, Abate | **12** Hija ya Wagane na Wajane 12-18.07 Kongamano la Damu Takatifu Mt. Veronika |
| **13** Dominika ya 15: Mwaka C Semina ya Uongozi (P) | **14** | **15** Mt. Bonaventura | **16** Bikira Maria wa Mlima Karmeli | **17** | **18** Kamati Tendaji Dekania | **19** **Jubilei Kuu: Dekania Mbezi Louis** |
| **20** Dominika ya 16: Mwaka C | **21** | **22** Sikukuu ya Mt. Maria Magdalene | **23** Mt. Brigita wa Sweden | **24** Misa kuombea Miito (Maaskofu, UMAWADA, MAJIDA, Masista..) | **25** Sikukuu ya Mt. Yakobo, Mtume | **26** Wat. Yoakim na Anna, wazazi wa B. Maria |
| **27** Dominika ya 17 Mwaka C **Mkutano Maalum HW Parokia** | **28** **Jubilei Kuu**: Vijana miaka 20 + 28.07 – 03.08 Hija Roma (ulimwengu) | **29** Mt. Martha | **30** Mt. Petro Krisogoni | **31** Mt. Inyasi wa Loyola | | |

| AGOSTI 2025 - Moyo Safi wa Bikira Maria | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | | | 03-11.08 Kupanda Mlima K'njaro – wanaume, familia, Maklero | | **1** Kuanza Novena kwa sikukuu ya Parokia | **2** Kamati Utekelezaji Dekania - Makabe |
| **3** Dominika ya 18: Mwaka C<br>Kipaimara Msumi | **4** Mt. Yohane Maria Vianney | **5** Kutabarukiwa Basilika la Mama Maria Mkuu<br>Mafungo, semina – Damu Azizi | **6** Kung'ara kwa Yesu Kristo | **7** | **8** Nane Nane - Wakulima<br>Bonanza WAWATA, Tabata | **9** Mt. Teresa Benedikta wa Msalaba<br>Kipaimara Mpiji Magohe |
| **10** Dominika ya 19 Mwaka C<br>**Kipaimara Mshikamano** | **11** | **12** | **13** 13-17.08 Kongamano la vijana taifa, Mbeya | **14** Mt. Maximilian Maria Kolbe | **15** Sherehe ya Kupalizwa Mbinguni Bikira Maria | **16** |
| **17** Dominika ya 20: Mwaka C | **18** | **19** | **20** | **21** | **22** Bikira Maria Malkia | **23** Mafungo, Semina UFATA (J) |
| **24** Dominika ya 21: Mwaka C | **25** Sikukuu ta Mt. Bartolome, Mtume | **26** | **27** Mt. Monika | **28** Mt. Augustino<br>Kuanza Novena ya Mt. Augustino | **29** Kufa shahidi Mt. Yohane Mbatizaji | **30** Ziara ya WAWATA, Visiga Seminari |
| **31** Dominika ya 22: Mwaka C | | | | | | |

| SEPTEMBA 2025 – Mateso saba ya Bikira Maria | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumapili | Jumatatu | Jumanne | Jumatano | Alhamisi | Ijumaa | Jumamosi |
| Hija ya UFATA na Jubilei: Australia - Roma | 1 | 2 | 3<br>Mt. Gregory Mkuu | 4 | 5<br>Maulidi<br>**Mt. Theresa wa Calcuta**<br>05-21.09 Kongamano la Kinabii, Karismatiki, Emaus | 6<br>**Sikukuu ya Dekania, Mt. Augustino - Makabe**<br>06-08.09 Hija ya SKAUTI Morogoro |
| 7<br>Dominika ya 23<br>Jubilei miaka 25, sikukuu, somo wa Wajane na Wagane – Mt. Monika | 8<br>Sikukuu ya kuzaliwa Bikira Maria | 9<br>Mt. Peter Claver | 10 | 11<br>Kamati Tendaji Dekania | 12<br>Jina Takatifu la Maria | 13<br>Mt. Yohane Krisostom<br>Hija, sikukuu ya Kutukuka kwa Msalaba, Pugu |
| 14<br>Dominika ya 24: Sikukuu ya Kutukuka kwa Msalaba | 15<br>Bikira Maria wa Mateso | 16 | 17 | 18<br>Mt. Joseph wa Kopertino | 19 | 20<br>Halmashauri Walei Dekania – Msumi<br>**Jubilei Kuu**: Wanasheria |
| 21<br>Dominika ya 25: Mwaka C | 22<br>Sikukuu Mt. Matayo, Mtume na Mwinjili | 23<br>Mt. Padre Pio wa Pietrelcina | 24 | 25<br>Hija kitaifa, Wazee na Wastaafu, Singida | 26<br>**Jubilei Kuu**: Makatekista 26-28 Sept. | 27<br>Mt. Vinsenti wa Paulo<br>-Kikao cha utendaji, viongozi Dekania na Kamati (J) |
| 28<br>Dominika ya 26: Mwaka C<br>Ndoa na Familia (Parokia) | 29<br>Wat. Mikaeli, Gabrieli na Rafaeli, Malaika Wakuu | 30 | | | | |

| OKTOBA 2025 - Rozari Takatifu | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | | | **1**<br>Mt. Theresia wa Mtoto Yesu<br>Jubilei ya Mapadre Jimbo | **2**<br>Wat. Malaika Walinzi | **3** | **4**<br>-Mt. Francis wa Asizi<br>-Mt. Theresia wa Mtoto Yesu – Upendo Group<br>-Kikao cha utendaji viongozi VMJ (J) |
| **5**<br>Dominika ya 27: Mwaka C<br>Mt. Maria Faustina Kowalska | **6** | **7**<br>Bikira Maria wa Rozari | **8**<br>**Jubilei Kuu**: Watawa, 8-9 Okt. | **9**<br>Mt. Denis | **10** | **11**<br>Mt. Yohane XXIII<br>Kamati Utekelezaji Dekania - Mageti |
| **12**<br>Dominika ya 28:<br>Mt. Margareta Maria Alakok (Mkuza) (Moyo Mt)<br>**Mkutano HW (J)** | **13** | **14**<br>Nyerere Day<br>- Hija ya UWAKA (J) Tegemeza Dada Wadogo Visiga | **15**<br>Mt. Theresa wa Avila<br>Kumb. Kutabarukiwa Kanisa Kuu la Mt. Yosefu Jimbo | **16**<br>Mt. Margarita Maria Alakok | **17** | **18**<br>-Sikukuu ya Mt. Luka, Mwinjili<br>-Rozari kuombea umoja na Amani duniani, Utoto - Msimbazi |
| **19**<br>Dominika ya 29: Uenezaji Injili, Umisionari<br>**Mkutano HW Parokia**<br>Mt. Paulo wa Msalaba | **20** | **21**<br>Mt. Gasapar del Bufalo | **22**<br>Mt. Yohane Paulo II | **23** | **24**<br>Mt. Anton Maria Klaret | **25**<br>**Warsha ya Waamini Jimbo** |
| **26**<br>Dominika ya 30: Mwaka C | **27** | **28**<br>Wat. Simon na Yuda Thadei, Mitume | **29** | **30** | **31**<br>**Jubilei Kuu**: Walimu wakatoliki<br>Hitimisho Jubilei miaka 200 ya kuzaliwa Kard. Lavigerie, Mshikamano | |

| NOVEMBA 2025 - Marehemu wa Toharani | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | 01-08.11 Hija Dodoma, Wana Damu Azizi ya Yesu Na 09-16.11 Mafungo, Semina | | | | | **1** Sherehe ya Watakatifu Wote |
| **2** Dominika ya 31: Kuwakumbuka marehemu wote **Mavuno Parokia** | **3** Mt. Martin de Porres | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** Hija UWAKA (J) Bagamoyo |
| **9** Dominika ya 32: Sikukuu – Kutabarukiwa Basilika la Laterani | **10** Mt. Leo Mkuu | **11** | **12** | **13** | **14** | **15** Semina za Kidekania HW (J) |
| **16** Dominika ya 33 -Kuwakumbuka maskini wote – CARITAS Day - UFATA Day (J) **Jubilei Kuu**: Wahitaji | **17** | **18** Kutabarukiwa Mabasilika na Petro na Paulo, Mitume | **19** | **20** Kamati Tendaji Dekania | **21** Kutolewa Bikira Maria Hekaluni | **22** Mt. Secilia **Shukrani ya MAVUNO (J)** **Jubilei Kuu**: Wanakwaya, 22-23.11 |
| **23** Sherehe ya B. W. Yesu Kristo Mfalme - Siku ya Vijana ulimwenguni | **24** | **25** | **26** | **27** | **28** Mafungo ya wana Moyo Mt wa Yesu kwa Hija Bagamoyo | **29** Hija na Mafungo ya HW (J) - Bagamoyo |
| **30** Dominika ya 1 ya Majilio Mwaka A | | | | | | |

| DESEMBA 2025 - Kuzaliwa Bwana | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Jumapili** | **Jumatatu** | **Jumanne** | **Jumatano** | **Alhamisi** | **Ijumaa** | **Jumamosi** |
| | **1**<br>Mt. Andrea, Mtume<br>Mwny. Anuatite | **2** | **3**<br>Mt. Francis Ksaveri | **4** | **5** | **6**<br>-Hija, Misa shukrani Upendo Group, Bagamoyo<br>-Hija WAWATA (J), Bagamoyo |
| **7**<br>Dominika ya 2 ya Majilio Mwaka A | **8**<br>Sherehe ya Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili (Imakulata)<br>- Nadhiri za Daima, Jubilei Dada Wadogo, Mt. F.A, Mbagala | **9**<br>Uhuru Tanganyika<br><br>Kamati Tendaji Dekania | **10** | **11** | **12**<br>Bikira Maria wa Guardalupe | **13**<br>Mt. Lusia<br><br>Mkutano Mkuu Halmashauri W. Dekania – Tegeta A |
| **14**<br>Dominika ya 3 ya Majilio<br>Mt. Yohane wa Msalaba<br><br>**Jubilei Kuu**: Wafungwa | **15** | **16** | **17** | **18** | **19** | **20** |
| **21**<br>Dominika ya 4 ya Majilio Mwaka A | **22** | **23** | **24**<br>Mkesha wa Noeli Majilio | **25**<br>Sherehe ya Noeli, Kuzaliwa Bwana | **26**<br>Sikukuu Mt. Stefano, Shahidi | **27**<br>Sikukuu Mt. Yohane, Mtume na Mwinjili<br>- Wat. Watoto Mashahidi, Utoto Mt<br>- Misa ya Ufukweni Vijana |
| **28**<br>Sherehe ya Familia Takatifu | **29** | **30** | **31**<br>Mt. Silvester | | | |

# VIPAUMBELE VYA PAROKIA 2025

**Taarifa na mwendelezo wa utekelezaji 2025**

**A: MIUNDOMBINU**

**1. Mipango na vipaumbele vya muda mfupi:**

| Na | Kipaumbele | Maelezo | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Kanisa: umaliziaji upakaji rangi. Pia uboreshaji milango ya Kanisa | Upakaji rangi nje ya Kanisa | Umeanza, utaendelea |
| 2 | Uboreshaji wa choo cha Parokia | Kuziba uwazi upande wa wanaume | Umeanza, utaendelea |
| 3 | Kuboresha landscaping, kuboresha mazingira yake. | Upandaji miti, maua | Umeanza, utaendelea eneo la nyumba ya mapadre |
| 4 | Kuboresha mfumo wa ulinzi Parokiani. | Kuongeza kamera Sakristia, mlango wa kaskazini; ujenzi wa uzio eneo la Kanisa. | Bado, utaendelea |
| 5 | Kukamilisha utengenezaji madawati (uboreshaji baadhi ya madawati). | Bado 11 mapya na 12 ya mbele. | Bado, utaendelea |
| 6 | Ujenzi wa sehemu ya kufulia vitu vitakatifu (Sacrarium). | Kuainisha eneo na aina ya ujenzi (masterplan) | Utafanyika |
| 7 | Kuweka marble yaani vigae na kuchora picha ya somo wa Parokia mbele ya Kanisa | **Kuanza** | **Umekamilika** |
| 8 | Kuongeza urembo kwa chuma zinazozunguka pembeni ya kanisa (corridor). | Kuendelea | Bado, utaendelea |
| 9 | Ufuatiliaji wa hati ya viwanja vya Parokia | Kuendelea | Kukamilisha |
| 10 | Uwekaji feni Kanisani | - | Kuanza |
| 11 | Ujenzi wa shedi kwa ajili ya mikutano, mafundisho | - | Kuanza |

**2. Mipango na vipaumbele vya muda mrefu:**

| Na | Kipaumbele | Maelezo | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya mapadre. | Ujenzi wa kuta, upauaji na mifumo ya maji na umeme umekamilika | Kukamilisha na kuzindua |
| 2 | Ujenzi wa Groto, chumba cha kuabudia Ekaristi daima na msalaba wa Jubilei. | Ukamilishaji michoro na gharama. | Utaendelea |
| 3 | Ujenzi wa ofisi za Paroko Msaidizi, Kamati Tendaji, Makatekista na VMJ – jengo la huduma. | Kukamilisha masterplan iongoze ujenzi | VMJ bado havina ofisi |
| 4 | Uboreshaji wa ukumbi kwa matumizi ya Parokia na kuwa chanzo cha mapato. | Upembuzi, uboreshaji unaendelea | Kamati ya Ujenzi inafanyia kazi (tathmini). |
| 5 | Ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la kanisa | Utaanza kutegemeana na masterplan | Inasubiri masterplan ya Parokia |
| 6 | Ujenzi wa nyumba ya Masista | Masterplan | Kukamilisha masterplan |
| 7 | Ujenzi wa shule ya awali na zahanati | Masterplan | Kukamilisha masterplan |
| 8 | Ujenzi wa mabanda ya biashara pande za barabara za pembeni kwa eneo la kanisa | Masterplan | Kukamilisha masterplan ya Parokia |

## B: KIROHO/KITUME

### 1. Mipango na vipaumbele vya muda mfupi:

| Na | Kipaumbele | Maelezo | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Kuunda, kuimarisha utendaji wa Kamati za kikatiba na za kitaaluma. Kuongeza vijana | Kuunda mpya na kuendelea na utekelezaji majukumu yake | Umefanyika, Baadhi ya Kamati kuimarishwa |
| 2 | Kuimarisha utendaji wa vyama na mashirika ya kitume. | Mipango yao – vikao na miradi | Inaendelea |
| 3 | Uandaaji na ushiriki wa vikao, mikutano – Halmashauri ngazi zote, Vyama, Mashirika na Kamati (uundaji wa Kamati katikaJumuiya na Kanda). | Kuendelea | Inaendelea |
| 4 | Ununuaji wa vifaa vya liturujia, altareni na mavazi ya Misa kwa mapadre na watumishi. | Utaendelea | Inaendelea kwa mwongozo wa mababa |
| 5 | Kuhamasisha katika uimbaji kwa kuanzisha Kwaya mpya walau kuimba mara moja kwa mwezi na watumishi wa zamani kutumikia baadhi ya Misa hasa za asubuhi na baadhi ya matukio | Imeanza, changamoto mahudhurio | Hamasa kuendelea na kuingia katika utekelezaji |
| 6 | Kuweka masalia ya Mt. Yohane Paulo II na kuzindua nyumba ya Mapadre | Mipango kuanza | Mtarajio kufanyika katika Sikukuu ya Somo wa Parokia 10.08.2025 |
| 7 | Kukamilisha taratibu za ujio wa masista kusaidia eneo la malezi na mafundisho ya watoto | Mipango inaendelea | Kukamilisha mawasiliano na makubaliano na Shirika la Masista wa Shirika la Mabinti wa Maria Kipalapala Tabora. |

### 2. Mipango na vipaumbele endelevu:

| Na | Kipaumbele | Maelezo | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 1 | Kampeni ya kuimarisha ndoa na familia (mkazo kutembelea na kuhamasisha wasio na ndoa) – semina kwa kuimarisha ndoa na familia kwa wakubwa (uhuishaji ndoa), vijana na watoto. | Kuendelea, mapadre kutembelea familia na Jumuiya | Kamati ya Ndoa na Familia na Kamati ya Malezi, Familia na Afya zimeundwa, kufuatilia<br>Waliosoma kozi ya UFATA Parokia kuungana na Kamati hizo, wengine kusoma kozi hiyo. |
| 2 | Kuimarisha utendaji wa Jumuiya Ndogo Ndogo – semina za Uongozi katika Halmashauri ya Walei na Uimarishaji Jumuiya Ndogo Ndogo za Kikristo. | Kuendelea | - Semina kuendelea |
| 3 | Kuendesha semina na mafungo ya kuimarisha imani (Kamati Tendaji, Halmashauri, Vyama na Mashirika ya Kitume na waamini wote). | Kuendelea | -Semina za utoaji (zaka), uongozi na maana ya mavuno<br>Kuunda Kamati ya Mavuno |
| 4 | Ulipaji zaka - utoaji sahihi wa zaka (utaratibu na uhamasishaji). | Kuendelea – Kamati imeboreshwa | Hamasa inaendelea kujisajili na kulipa kidigitali |
| 5 | Kufanya hija za kiparokia – Pugu, Bagamoyo, Mbagala Msalabani au kwingineko mara moja kila nusu ya mwaka. | Kuendelea | Mwaka 2024 haikufanyika Hija ya Kiparokia. 2025 zinapangwa hasa kuzingatia Jubilei Kuu 2025 |
| 6 | Kulea vipaji vya watoto mfano muziki mtakatifu – utunzi, usomaji nota na upigaji wa ala. | Kuendelea | Kuendelea kwa msukumo zaidi |
| 7 | Uwekaji na utunzaji kumbukumbu za Parokia kwa vizazi vijavyo: Kupitia mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kuweka picha za maparoko walioongoza Parokia | --- | Kuanza 2025 |

## RATIBA YA USAFI, USIMAMIZI NA VIPAJI: 01.01.2025 – 31.12.2025

### MWAKA WA JUBILEI KUU

| TAREHE | DOMINIKA/SIKUKUU/ SHEREHE | JUMUIYA / CHAMA CHA KITUME | |
|---|---|---|---|
| | | MISA 1 | MISA 2 |
| | MKESHA WA MWAKA MPYA | UWAKA | |
| 01/01/2025 | Maria Mtakatifu Mama wa Mungu | WAWATA | |
| 05/01/2025 | Sherehe Tokeo la Bwana - Epifania | Mt. Gaspar del Bufalo | Mt. Yohane Maria Vianney |
| 12/01/2025 | Sikukuu ya Ubatizo wa Bwana | Mt. Silvester | Mt. Yakobo Mtume |
| 19/01/2025 | Dominika ya 2 Mwaka C | Mt. Stefano Shahidi | Mt. Yohane Mtume na Mwinjili |
| 26/01/2025 | Dominika ya 3 – NENO la Mungu | Mt. Yuda Thadei | Mwny. Anuarite |
| 02/02/2025 | Si'kuu ya Kutolewa Bwana Hekaluni | Familia Takatifu | Mt. Martin de Porres |
| 09/02/2025 | Dominika ya 5 Mwaka C | Mt. Joseph Mfanyakazi | Mt. Kizito |
| 16/02/2025 | Dominika ya 6 Mwaka C | Mt. Mathias Mulumba | Moyo Mtakatifu wa Yesu |
| 23/02/2025 | Dominika ya 7 Mwaka C | Mt. Isidori Mkulima | Mt. Petro Mtume |
| 02/03/2025 | Dominika ya 8 Mwaka C | Mt. Rafaeli Malaika Mkuu | Mt. Denis |
| 05/03/2025 | Jumatano ya MAJIVU | Karismatiki Katoliki na Moyo Mt wa Yesu (Shirika) | |
| 09/03/2025 | Dominika ya 1 Kwaresma Mwaka C | Mt. Joseph wa Kopertino | Mt. Francis wa Asizi |
| 16/03/2025 | Dominika ya 2 Kwaresma Mwaka C | Kristo Mfalme | Mt. Monika |
| 19/03/2025 | Sherehe ya Mt. Yosefu, Mume wa Bikira Maria | UWAKA | |
| 23/03/2025 | Dominika ya 3 Kwaresma Mwaka C | Mt. Paulo Mtume | Mt. Paulo wa Msalaba |
| 25/03/2025 | Sherehe kupashwa habari ya kuzaliwa Bwana | WAWATA | |
| 30/03/2025 | Dominika ya 4 Kwaresma Mwaka C | Mt. Timotheo | Mt. Anna |
| 06/04/2025 | Dominika ya 5 Kwaresma Mwaka C | Mt. Bernadeta | Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni |
| 13/04/2025 | Dominika ya Matawi – Mateso ya Bwana Mwaka C | Mt. Secilia | Mt. Theresa wa Avila |
| 17/04/2025 | ALHAMISI KUU | Karismatiki Katoliki na Moyo Mt. wa Yesu (Shk.) | |
| 18/04/2025 | IJUMAA KUU | UWAKA | |
| 19/04/2025 | JUMAMOSI KUU - MKESHA | UWAKA | |
| 20/04/2025 | UFUFUKO WA BWANA - PASAKA | WAWATA | VIWAWA |
| 21/04/2025 | Jumatatu ya Pasaka | WAWATA / VIWAWA | |
| 27/04/2025 | Dom. 2 Pasaka - Huruma ya Mungu | Mt. Anton wa Padua | Mt. Augustino |
| 01/05/2025 | Mei Mosi - Mt. Yosefu Mfanyakazi | UWAKA | |
| 04/05/2025 | Dominika ya 3 Pasaka Mwaka C | Mt. Maximilian Kolbe | Mt. Perpetua |
| 11/05/2025 | Dominika ya 4 Pasaka Mwaka C | Mt. Yohane Krisostom | Mt. Rita wa Kashia |
| 18/05/2025 | Dominika ya 5 Pasaka Mwaka C | Mt. Yohane Mbatizaji | Mt. Gregory VII |
| 25/05/2025 | Dominika ya 6 Pasaka Mwaka C | Mt. Brigita wa Sweden | Mt. Padre Pio |
| 29/05/2025 | Alhamisi (siku 40 baada ya Pasaka) | | |
| 01/06/2025 | Sherehe ya Kupaa Bwana Mbinguni | Mt. Martha | Mt. Katarina wa Siena |
| 07/06/2025 | Kesha la Pentekoste | UWAKA | |
| 08/06/2025 | Sherehe ya Pentekoste | Mt. Maria Goretti | Kung'ara kwa Yesu Kristo |
| 15/05/2025 | Dominika ya Utatu Mtakatifu | Mt. Yohane Maria Vianney | Mt. Filipo Mtume |
| 22/06/2025 | Sherehe ya Mwili na Damu Takatifu ya Bwana Yesu Kristo | Mt. Yohane Mtume na Mwinjili | Mt. Yohane Paulo II |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 24/06/2025 | Sherehe Kuzaliwa Mt. Yohane Mbatizaji | WAWATA | |
| 27/06/2025 | Sherehe ya Moyo Mtakat. wa Yesu | Moyo Mtakatifu wa Yesu (Shk.) (Ijumaa) | |
| 29/06/2025 | Sherehe Watatakatifu Petro na Paulo Mitume | Mt. Yakobo Mtume | Mt. Gaspar del Bufalo |
| 06/07/2025 | Dominika ya 14 Mwaka C | Mwy. Anuarite | Mt. Silvester |
| 13/07/2025 | Dominika ya 15 Mwaka C | Mt. Martin de Porres | Mt. Stefano Shahidi |
| 20/07/2025 | Dominika ya 16 Mwaka C | Mt. Kizito | Mt. Yuda Thadei |
| 27/07/2025 | Dominika ya 17 Mwaka C | Moyo Mtakatifu wa Yesu | Familia Takatifu |
| 03/08/2025 | Dominika ya 18 Mwaka C | Mt. Petro Mtume | Mt. Joseph Mfanyakazi |
| 06/08/2025 | Sikukuu ya Kung'ara Bwana Yesu Kristo (Msimamizi wa Parokia) | Kuadhimishwa rasmi Dominika 10.08.2025 | |
| 10/08/2025 | Dominika ya 19 Mwaka C | Mt. Denis | Mt. Mathias Mulumba |
| 15/08/2025 | Sherehe ya Kupalizwa Mbinguni Bikira Maria | Lejio ya Maria na Bikira Maria Mki. Dhambi ya Asili | |
| 17/08/2025 | Dominika ya 20 Mwaka C | Mt. Francis wa Asizi | Mt. Isidori Mkulima |
| 24/08/2025 | Dominika ya 21 Mwaka C | Mt. Monika | Mt. Rafaeli Malika Mkuu |
| 31/08/2025 | Dominika ya 22 Mwaka C | Mt. Paulo wa Msalaba | Mt. Joseph wa Kopertino |
| 07/09/2025 | Dominika ya 23 Mwaka C | Mt. Anna | Kristo Mfalme |
| 14/09/2025 | Dominika ya 24 Mwaka C | Bikira Maria Mpalizwa Mbi. | Mt. Paulo Mtume |
| 21/09/2025 | Dominika ya 25 Mwaka C | Mt. Theresa wa Avila | Mt. Timotheo |
| 28/09/2025 | Dominika ya 26 Mwaka C | Mt. Augustino | Mt. Bernadeta |
| 05/10/2025 | Dominika ya 27 Mwaka C | Mt. Perpetua | Mt. Secilia |
| 12/10/2025 | Dominika ya 28 Mwaka C | Mt. Rita wa Kashia | Mt. Anton wa Padua |
| 19/10/2025 | Dominika ya 29 – Dominika ya Umisionari | Mt. Gregory VII | Mt. Maximilian Kolbe |
| 27/10/2025 | Dominika ya 30 Mwaka C | Mt. Padre Pio | Mt. Yohane Krisostom |
| 01/11/2025 | Sherehe ya Watakatifu Wote | WAWATA | |
| 02/11/2025 | Dominika 31 - Kuwakumbuka marehemu wote | Mt. Katarina wa Siena | Mt. Yohane Mbatizaji |
| 09/11/2025 | Dominika ya 32 Mwaka C | Kung'ara kwa Yesu Kristo | Mt. Brigita wa Sweden |
| 16/11/2025 | Dominika ya 33 Mwaka C | Mt. Filipo Mtume | Mt. Martha |
| 23/11/2025 | Sherehe ya Bwana Wetu Yesu Kristo Mfalme | Mt. Yohane Paulo II | Mt. Maria Goretti |
| 30/12/2025 | Dominika ya 1 ya Majilio Mwaka A | Mt. Gaspar del Bufalo | Mt. Yohane Maria Vianney |
| 07/12/2025 | Dominika ya 2 ya Majilio Mwaka A | Mt. Silvester | Mt. Yohane Mtume na Mwinjili |
| 08/12/2025 | Sherehe ya Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili | Lejio ya Maria na Bikira Maria Mki. Dhambi ya Asili | |
| 14/12/2025 | Dominika ya 3 ya Majilio Mwaka A | Mt. Stefano Shahidi | Mt. Yakobo Mtume |
| 21/12/2025 | Dominika ya 4 ya Majilio Mwaka A | Mt. Yuda Thadei | Mwny. Anuarite |
| 24/12/2025 | MKESHA WA NOELI | UWAKA | |
| 25/12/2025 | KUZALIWA BWANA - NOELI | WAWATA | VIWAWA |
| 26/12/2025 | Sikukuu ya Mt. Stefano Shahidi | VIWAWA | |
| 28/12/2025 | Watakatifu Watoto Mashahidi/ Misa ya Ufukweni | | |
| 28/12/2025 | Sherehe ya Familia Takatifu | Familia Takatifu | Martin de Porres |
| 31/12/2025 | Mkesha wa Mwaka Mpya 2026 | UWAKA | |

## MAPADRE WALEZI WA VYAMA, MASHIRIKA NA JUMUIYA ZA KITUME (VMJ) PAROKIA

| CHAMA | PADRE MLEZI |
|---|---|
| 1. Bikira Maria Mkingiwa Dhambi ya Asili<br>2. Lejio ya Maria<br>3. Karismatiki Katoliki<br>4. Moyo Mtakatifu wa Yesu | Padre Theodore Ouedraogo |
| 1. UWAKA<br>2. WAWATA<br>3. Wazee na Wastaafu<br>4. Mt. Vincent wa Paulo<br>5. Christian Professionnals of Tanzania (C.P.T.)<br>6. Couples for Christ (C.F.C.) - Utume wa Familia Katika Kristo | Padre Gilbert Bujiriri |
| 1. VIWAWA<br>2. UKWAKATA<br>3. Watumishi wa Altare (Alter boys)<br>4. Utoto Mtakatifu<br>5. T.Y.C.S/ T.M.C.S<br>6. Waseminari | Padre Venance Bharotota |

**Ufunguo:**

TMCS **-** Tanzania Movement of Catholic Students (Umoja wa Wanafunzi Wakatoliki Tanzania) -Vyuoni

TYCS - Tanzania Young Catholics Students - Shuleni

## UFUPISHO WA KALENDA YA MIKUTANO NA MATUKIO MENGINE

| MWEZI | MKUTANO WA HALMASHAURI YA WALEI PAROKIA | MATUKIO MENGINE – SEMINA, MAFUNGO, HIJA |
|---|---|---|
| Januari | | |
| Februari | Dominika 09.02 | |
| Machi | | - Mafungo WAWATA, 22.03<br>- Mafungo watoto, 31.03 |
| Aprili | | - Mafungo ya Kwaresma Parokia 01.04,<br>- Mafungo ya Vijana 12.04<br>- Kupokea sanamu ya Bikira Maria 05.04, na kuikabidhi 22.04)<br>- Utambulisho mafundisho ya UFATA 06.04 |
| Mei | | |
| Juni | Dominika 08.06 | - Semina Kamati ya Uinjilishaji, Jumamosi 21.06 |
| Julai | Mkutano Maalum H. Walei (P), Dominika 27.07 | - Hija na mafungo Parokia, Jumamosi 05.07<br>- Semina uongozi, Dominika 13.07 |
| Agosti | | - Novena ya Parokia, 01- 09.08<br>- Sakramenti: Kipaimara, Ndoa, Dominika 10.08<br>- Masalia ya Mt. Yohane Paulo II, Altareni<br>- Uzinduzi nyumba ya mapadre, 10.08 |
| Septemba | | - Semina – ndoa na familia, Dominika 28.09 |
| Oktoba | Dominika, 19.10. | |
| Novemba | | - Mavuno Parokia, Dominika 02.11 |
| Desemba | | |

## NIA ZA SALA ZA KILA SIKU

1. Dominika - Ufufuko wa Bwana Yesu
2. Jumatatu - Roho Mtakatifu
3. Jumanne - Malaika
4. Jumatano - Mt. Yosefu
5. Alhamisi - Ekaristi Takatifu
6. Ijumaa - Ibada ya Moyo Mtakatifu wa Yesu
7. Jumamosi - Maria Bikira Mama wa Rozari

## SIKUKUU NA MAOMBI YA MISA ZA WASIMAMIZI WA JUMUIYA NA KANDA 2025

Msimamizi wa Parokia - Kung'ara kwa Yesu Yesu Kristo: 06 Agosti

| KANDA | JUMUIYA | SIKUKUU HALISI | SIKU YA MISA |
|---|---|---|---|
| **A:** Mt. Basili Mkuu 02 Januari *Vipaji Kanisani 23.02* | Mt. Brigita wa Sweden | 23 Julai | 26.07 |
| | Mt. Katarina wa Siena | 29 Aprili | 03.05 |
| | Kung'ara kwa Yesu Kristo | 06 Agosti | |
| | Mt. Martha | 29 Julai | |
| **B:** Mt. Francis Ksaveri 03 Des. **06.12.25** | Mt. Filipo Mtume | 03 Mei | 03.05 |
| | Mt. Gaspar del Bufalo | 21 Oktoba | 22.10 |
| | Mt. Maria Goretti | 06 Julai | 05.07 |
| | Mt. Yohane Maria Vianney | 4 Agosti | 09.08 |
| | Mt. Yohane Paulo II | 22 Oktoba | 25.10 |
| **C:** Mt. Veronika 12 Julai **09.07.25** | Mt. Silvester | 31 Desemba | 31.12 |
| | Mt. Stefano Shahidi | 26 Desemba | 29.11 |
| | Mt. Yakobo Mtume | 3 Mei | 25.07 |
| | Mt. Yohane Mtume na Mwinjili | 27 Desemba | 03.01.2026 |
| | Mt. Yuda Thadei | 28 Oktoba | 25.10 |
| **D:** Mt. Maria Magdalena 22 Julai **26.07.25** | Mwenyeheri Anuarite | 01 Desemba | 06.12 |
| | Familia Takatifu | 28 Desemba | 29.11 |
| | Mt. Martin de Porres | 03 Novemba | 08.11 |
| **E:** Mt. Inyasi wa Loyola 31 Julai **02.08.2025** | Mt. Joseph Mfanyakazi | 01 Mei | 03.05 |
| | Mt. Kizito | 03 Juni | 07.06 |
| | Mt. Mathias Mulumba | 03 Juni | 07.06 |
| | Moyo Mtakatifu wa Yesu | 27 Juni | 28.06 |
| **F:** Bikira Maria wa Lurdi 11 Februari | Mt. Isidori Mkulima | 15 Mei | 17.05 |
| | Mt. Petro Mtume | 29 Juni | |
| | Mt. Rafaeli Malaika Mkuu | 29 Septemba | 27.09 |
| **G:** Mt. Thomas wa Akwino 28 Januari *Vipaji Kanisani 02.02.25* | Mt. Denis | 09 Oktoba | |
| | Mt. Francis wa Asizi | 04 Oktoba | 04.10 |
| | Mt. Joseph wa Kopertino | 18 Septemba | |
| | Kristo Mfalme | 23 Novemba | 22.11 |
| **H:** Mt. Stefano 26 Desemba | Mt. Monika | 27 Agosti | |
| | Mt. Paulo Mtume | 29 Juni | 28.06 |
| | Mt. Paulo wa Msalaba | 19 Oktoba | 18.10 |
| | Mt. Timotheo | 26 Januari | |
| **I:** Mt. Benedikto 11 Julai | Mt. Anna | 26 Julai | 26.07 |
| | Mt. Bernadeta | 15 Aprili | 26.04 |
| | Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni | 15 Agosti | 16.08 |
| | Mt. Secilia | 22 Novemba | 22.11 |
| | Mt. Theresa wa Avila | 15 Oktoba | 18.10 |
| **J:** Mt. Maria Faustina Kowalska 05 Oktoba **11.10.25** | Mt. Antoni wa Padua | 13 Juni | 16.06 |
| | Mt. Augustino | 28 Agosti | 06.09 |
| | Mt. Maximilian Kolbe | 14 Agosti | 16.08 |
| | Mt. Perpetua | 7 Machi | 14.06 |
| | Mt. Rita wa Kashia | 22 Mei | 24.05 |
| **K:** Mt. Theresa wa Calcutta 5 Sept. **06.09.2025** | Mt. Gregory VII | 25 Mei | 26.05 |
| | Mt. Padre Pio | 23 Septemba | 27.09 |
| | Mt. Yohane Krisostom | 13 Septemba | 13.09 |
| | Mt. Yohane Mbatizaji | 24 Juni (Kuz); 29 Ag. (Kuf) | 28.06 |

**Angalizo**: Thibitisha tarehe ya maombi ya Misa angalau siku nane kabla kwa upatikanaji wa mapadre na kutangazwa Dominika moja kabla.

## KUMBUKUMBU YA BAADHI YA MATUKIO YA KIPAROKIA MWAKA 2024



Wanaparokia katika maandamano ya Sherehe ya Mwili na Damu ya Bwana Yesu Kristo wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Shirika, Pd. Gilbert Bujiriri MAfr., 02.06.2024



Mapadre na Masista walioshiriki adhimisho la Misa katika sikukuu ya Dekania 31.08.2024



Baba Provincial, Pd. Oswald Mallya (wa nne kulia) alipotembelea Parokia na kuadhimisha 21 Julai 2024



Baba Dekano, Pd. Sylvester Msemea OCD baada ya kutoa Kipaimara katika picha na Paroko Pd. Gilbert Bujiriri MAfr na Kamati Tendaji Parokia, 12.10.2024



Wanaparokia walishiriki kilele cha Kongamano la tano la Ekaristi Takatifu Kitaifa katika Uwanja wa Uhuru, 15.09.2024



Wana Undugu Association (Marafiki wa Wamisionari wa Afrka) wakiwa katika Mkutano Parokiani, 17.02.2024



Wanaparokia walishiriki Misa ya kuwakaribisha wanafunzi wa Pre-First Phase Formation House, Mshikamano, 14.09.2024



Kwaya ya Mt. Secilia kutoka Parokia ya Mongo la Ndege wakiinjilisha Parokiani, 22 Sept. 2024.



Adhimisho la Misa ya Mavuno Parokia na Pd. Patrice Ndemasi, 10 Nov. 2024.



Wana Moyo Mtakatifu wa Yesu wakirudia kiapo katika Sherehe ya Bwana Wetu Yesu Kristo Mfalme, 24.11.2024 mbele ya Paroko, Pd Gilbert Bujiriri



Mapadre Wamisionari wa Afrika, Masista wa Bibi Yetu wa Afrika (MSOLA) na Wana Undugu katika picha ya pamoja baada ya Adhimisho la Misa kusherehekea Lavigerie Day, 30.11.2024



Pd. Erasto Kamugisha (katikati) akiwa na Pd. Theodore Ouedraogo na Pd. Francis Xavier Angkosaala katika adhimisho la Misa ya siku ya UWAKA Parokia, 07.12.2024



Baba Askofu Mkuu, Mhashamu Sana Jude Thaddeaus Ruwa'ichi OFMCap akibariki matawi akiambatana na Paroko, Pd. Protogene Rugwizandekwe MAfr. Katika Dominika ya Matawi, 24.03.2024



Baba Askofu Mkuu, Mhashamu Sana Jude Thaddeaus Ruwa'ichi OFMCap akiwa pamoja na mapadre na Utoto Mtakatifu baada ya Adhimisho la Misa ya Matawi 24.03.2024






Mapadre na wana Dekania wakifuatilia nyimbo za Utoto Mtakatifu katika sikukuu ya Dekania Parokiani Mshikamano 31.08.2024



Utoto Mtakatifu kutoka Parokia za Dekania wakiimba wimbo maalum wa Mt. Augustino



UKWAKATA Parokia wakiimba katika Tamasha la Kwaya Dekania katika sikukuu ya Dekania 31.08.2024



Baba Dekano, Pd. Sylvester Msemwa, OCD akipanda mti wa kumbukumbu kwa kushirikiana na UWAKA na kuwakabidhi kuutunza



Baba Paroko na Makamu Mkuu wa Shirika la Wamisionari wa Afrika Kanda (Province) ya Afrika Mashariki, Pd. Gilbert Bujiriri, MAfr. akipanda mti wa kumbukumbu kwa kushirikiana na WAWATA ambao walikabidhiwa kuutunza



Baadhi ya watoto waliopokea Sakramenti ya Ekaristi, Komunio ya kwanza 01.09.2024



Wanaparokia wanajitoa kwa njia mbalimbali na shukrani kwa maendeleo ya Kanisa






Jubilei Kuu ya Ukristo Desemba 2024 – Desemba 2025

Padre Venance akifafua uhusiano wa Mt. Maria Faustina Kowalska na Huruma ya Mungu katika Misa ya Kanda 05.10.2024

